

Seminar

Lijue Kanisa la Kristo

June 24-27, 1997

Seminar – Kanisa la Kristo

June 24-27, 1997

<u>Masomo</u>	<u>Ukarasa</u>
1. Mafundisho Potofu Katika Kanisa - Robert Stapleton	03
2. Mwanzo Wa Kanisa - Amos Kisulumi	07
3. Kanisa Linaloteseka - B.J.M. Kulanga	09
4. Walimu Wa Uongo Kanisani - Robert Stapleton	11
5. Je, Biblia Ndiyo Yenye Mamlaka Katika Mwongoza Wa Biblia? - Heath Stapleton	13
6. Kazi Ya Kanisa - Edson J. Mwalugamba	15
7. Kanisa Na Ushirika Na Madhehebu? - Robert Stapleton	16
8. Kielelezo Cha Kanisa La Agano Jipyा - Heath Stapleton	18
9. Sababu Zinazofanya Kanisa Likue - Boaz Kasiba	20
10. Kanisa Na Nidhamu - Robert Stapleton	22
11. Kanisa La Kiaskari - Heath Stapleton	26
12. Tunajua Sisi Ni Kanisa La Bwana Kwa Sababu.... - Robert Stapleton	28

Mafundisho Potofu Katika Kanisa

Utangulizi

1. Kuna uasi mwingi ndani ya kanisa siku hizi.
 - a. Neno lenyewe la kiingereza “heresy” humaanisha “maoni maelezo yanayoleta faraka”.
 1. Neno hilo linatumika kufanana na neno “madhehebu” linalopatikana katika Mdo. 24:5, 14.
 2. Wale ambao wanaunga mkono uasi mbali mbali unaojitokeza ndani ya kanisa huitwa kwa kiingereza “heretics” (wapingaji).
 - a. Somo letu la leo litasaidia kuona baadhi ya upingaji huo na kuona namna ya kupinga.
- I. Maasi (upingaji) yalitabiriwa na Kristo na mitume.
- a. Kristo alionya juu yake, Mt. 7:15; 24:11, 24.
 - b. Petro alitabiri uasi wa kutisha, 2 Pet. 2:1.
 - c. Paulo alibashiri hivyo Efeso, Mdo. 20:29.
 - d. Walitajwa pia kama roho zidanganyazo, 1 Tim. 4:1.
- II. Baadhi ya maasi au mafundisho ya uongo yameonyeshwa.
- a. Dini ya Kiyahudi.
 1. Desturi ya Agano la Kale ya kutahiri ni ushahidi katika kundi hilo, Mdo. 15:1.
 - a. Paulo na Barnaba hawakukat aa kulishughulikia jambo hili, Mdo. 15:2; Gal. 2:3-5.
 - b. Petro aliliita kongwa lisilochukulika, Mdo. 15:10.
 - c. Dini ya kiyahudi ilipindua nafsi za watu, Mdo. 15:24; Gal. 5:2-4.
 2. Vyombo vya muziki ni maasi ya kiyahudi -yanaleta faraka.
 - a. Watu lazima wategemee Agano la Kale kama wanataka kuyadumisha hayo- “Daudi”.
 - b. Vyombo vya muziki vimepigwa marufuku katika Agano Jipy, Efe. 5:19; Gal. 1:8.
 - c. Wakatoliki wana mamlaka hayo hayo kutumia uvumba, Kut. 30:7-8.
 - d. Wasabato nao wanawenza kudai mamlaka kwa ajili ya Sabato, Kut. 20:8; Gal. 4:10,11; Kol. 2:14-16.
 3. Kurudi kwa Wayahudi na kuanzisha tena utaratibu wao wa maasi ya Kiyahudi - premillennialism.
 - a. Ahadi ya nchi ilitimizwa, Neh. 9:7, 8; Yos. 21: 43-45.
 - b. Leo hapana tofauti kati ya myahudi na mtaifa, Rom. 10:12; Gal. 3:28.
 - c. Taifa la Israeli haliwezi kuunganika liwe moja tena, Yer. 19:11.
 - b. Maasi (upingaji) ya ufufuo.
 1. Hakuna ufufuo, 1 Kor. 15:12.
 - a. Hili lingeangamiza msingi wa ukristo, 1 Kor. 15:13-19.
 2. Ufufuo umekwisha kupita, 2 Tim. 2:16-18.

- a. Hili ni swala muhimu ambalo linweza kuangusha imani ya wengi,
2 Tim. 2:18; 1 Tim. 1:19-20.
- 3. Kufufuka kuwili-ufufuo mmoja kwa ajili ya watakatifu na mwingine
kwa wenyе dhambi.
 - a. Ona, 1 Thes. 4:15-17.
 - b. Ufufuo mmoja kwa wote, Mdo. 24:15.
 - c. Hukumu kwa wote siku ya mwisho, Yn. 11:24; 12:48.
- c. Kuamini kudumu hali ya kidunia (materialism).
 - 1. Utawala wa kidunia wa Kristo katika Yerusalem.
 - 2. Lieleweke kwamba Ufalme wa Kristo si wa vitu vya muda, Yn. 18:36.
 - 3. Nadhania hiyo inavunja tumaini la wamataifa, Mdo. 15:13-17.
- d. Ufisadi.
 - 1. Huo ulikuwa ni maasi ya Wanikolai, Ufu. 2:6, 15.
 - 2. Pia maasi ya Wabalaamu na Wayezebeli, Ufu. 2:14-20.
 - 3. Hao watawajuia watu nje ya Ufalme wa Mungu, Gal. 5:19-21.
- e. Kuamini katika kutokea vitu kwa mabadiliko (evolution) katika wale
wasio na imani kwa Mungu.
 - 1. Kama imani hiyo itakubaliwa mtu hawezи kuamini Biblia.
 - a. Biblia inathibit isha uumbaji wa moja kwa moja, Mwa. 1:26-27; Mwa. 2:7.
 - 2. Biblia inafundisha kwamba mwanadamu aliumbwа akiwa mkamilifu na
akaanguka, sio alibadilika hatua kwa hauta katika muda wa miaka
mamilioni.
 - a. Haiwezekani kuamini katika hali zote mbili-mwanadamu kama
aliumbwа au alitokea kwa mabadiliko hayo.
 - 3. Kama mwanadamu anatokana na mzazi wa zamani ambaye alikuwa
mnyama (hayawani), yaani alaumiwe afanyapo mambo yasiyo maadili
ya binadamu na anafanya kama mnyama?
 - 4. Haiwezekani kukubadilika kwamba Mungu aliumba kwa njia ya
mabadiliko. (Theistic Evolution), Kut. 20:10-11.
- f. Talaka na ndoa ya pili.
 - 1. Yesu alitoa sababu moja tu maalum (uasherati) ndio inayoruhusu
kutaliki na kuoa tena, Mt. 19:9.
 - a. Mt. 19:9, si sehemu ya Agano la Kale, Yn. 8:4,5; Wal. 20:10.
 - b. Zote zipo chini ya sheria ya Kristo, Mk. 16:15,16; Mt. 28:18-20.
 - 1) Hapa maelekezo kwa aliyepotea yamejumlishwa.
 - c. Sheria ipi ilihuishiwa katika, Mt. 19:5.
 - 1) Angalia kwa makini, Mk. 6:17,18.
 - 2) Inawezekana sheria ya nchi huafiki aina fulani ya ndoa, lakini
Mungu anakataa kuafiki (mfano: ndoa ya wawili).
- g. Kanisa moja kuonekana kuwa ni zuri tu kama lingine.
 - 1. Udhehebu haujawahi kamwe kutimiza ukristo ya kweli wa Agano Jipya.
 - a. Masharti maalum ya kuingia katika madhehebu sio mambo muhimu ya
kuwa Mkristo.
 - 2. Kuwa mfuasi wa dhehebu fulani si sawa na kuwa Mkristo.
 - 3. Kuwa mfuasi wa kanisa (lenyewe) ni kuwa Mkristo.

- a. Kanisa hilo ni mwili wa Kristo, Kol. 1:18.
- b. Kristo ni Mwokozi wa mwili, Efe. 5:23.
 - 1) Kuwa katika mwili ni kwa katika kanisa.
- c. Kuwa katika Kristo ni kuwa katika hali ya wokovu, 2 Tim. 2:10.
- d. Hatua zinazompa mtu wokovu ndizo zinazomfanya mtu awe mfuasi wa kanisa.
 - 1) Bwana humwongeza katika kanisa, Mdo. 2:47.
 - 2) Kanisa ni jamaa ya Mungu, Gal. 6:10.
 - 3) Kuokolewa mtu lazima azaliwe kwa mara ya pili kwa mzao wa kiroho, Yoh. 3:3-5.
 - 4) Mtu amezaliwa na Mungu kwa kuwa mzaliwa mpya.
 - 5) Huku kuzaliwa kunamfanya tu aingie kaitka familia (jamaa) ya Mungu, kanisa.
 - 6) Kwa kuwa kanisa linaokoa pia, ni salama juhitimishe kwamba kuokolewa ni kuwa katika kanisa hilo.
- e. Kuwa mkristo ni kuwa mfuasi wa Kristo.
 - 1) Hakuna mtu aliyemfuasi wa kristo katika madhehebu.
 - 2) Paulo aliwambia Wakorintho wamfuate kama yeye alivyomfuata Kristo, 1 Kor. 11:1.
 - 3) Kamwe Paulo hakufuata madhehebu.
 - 4) Mitume walihubiri injili ile ile, na kutangaza laana ya mbiguni juu ya wale ambao wangehubiri injili nyingine, Gal. 1:6-9.
- f. Kila kundi (taasisi) ni matokea ya mafundisho.
 - 1) Kila jumuiya (shirika) imeundwa na mafundisho maalum kwa ajili yao yenye.
 - 2) Na Kanisa la Bwana ndivyo lilitivo, Lk. 8:11.
 - a) Kwa sababu kila mbegu hutokana na mmea wa aina yake, kama neno la Mungu tu litahubiriwa, ni Kanisa la Kristo tu litalozaliwa.
 - b) Mengi ya migawanyiko ya kididni duniani ni matokeo ya mafundisho ambayo watu hufundisha lakini Bwana wetu, mitume hawakufundisha hivyo.
 - (1) Mwanadamu anahitaji kuzingatia maonyo ya 2 Yoh. 9.
- h. Mafundisho ya umoja katika tofauti.
 - 1) Wale wanaoshikiria maoni haya waone sehemu zinazohusu “ushirika katika tofauti”.
 - 2) Ni mafundisho kwamba “mafundisho” si muhimu.
 - a) Ni ile imani kwamba kweli inaweza kuchanganywa na makosa na bado ikawa inampendeza Mungu, 1 Tim. 6:20.
 - 3) Kristo alikuja kuvunja kazi za Shetani, 1 Yoh. 3:8.
 - a) Je, Udhehebu ni kazi ya Kristo?
 - (1) Kama ndiyo, kwa nini aliombea umoja katika Yoh. 17?
 - b) Kuna mambo mengi ambayo wakristo hawawezi kuyashiriki.
 - (1) Kwamba mtu huokolewa aaminipo tu, Yoh. 3:5.
 - (2) Kwamba Mungu anaweza kufurahi watu wanapokuwa wamegawanyika katiak mafundisho na matendo, Yn. 17:20, 21;

1 Kor. 1:10-13.

- (3) Hatuwezi kuombea mafanikio ya juhudini ya kidini na mahali ambapo mpango wa wokovu hauhubiriwi kwa watu, Mk. 16:16; Mdo. 2:28; Gal. 3:26,27.
- (4) Hatuwezi kuwasaidia na kuwafariji (katika mwenendo wao) maadui, Gal. 1:6-8.
- c) Tusiwe tayari kuchukua maelezo ya watu na kuyafanya ni mamlaka ya dini.
- i. Hakuna haja ya kuwa na wazee (wa kanisa) siku hizi.
 - 1) Wengine husema majukumu ya wazee yaliokomea wakati wa uvuvio ulipokoma.
 - a) Lakini hakuna mafundisho yanayothibitisha hilo katika Agano Jipyä.
 - 2) Kadiri muda unavyoendelea, wazee watahitajiwa kuangalia kazi ya kufundisha, Mdo. 20:28; 1 Tim. 5:17; Ebr. 13:7; 1 Tim. 3:5.
 - a) Kama wazee walikuwa wameondolewa ni nani angetimiza hayo yaliyoamuriwa katika sehemu hizo?
 - 3) Daima kanisa litahitaji kuchungwa.
 - a) Kwa hiyo, daima kutahitajika kiwako wazee, 1 Pet. 5:2.
 - 4) Sifa za kazi ya mzee wa kanisa hazikutegemea mambo ya miujiza.
 - 5) Wajibu (uangalizi) huo utaendelea mpaka kuja kwa mara ya pili, 1 Pet. 5:4.

Mwisho

1. Ni vizuri kutahadharishwa kuhusu mafundisho potofu ndani ya kanisa siku hizi.
2. Lazima tuwe waangalifu -hatuwezi kufuata namna ya mafundisho, Efe. 4:14.

Asante : Robert Stapleton

Mwanzo Wa Kanisa

Yer. 31:31; 32:31, Mt. 16:18.

Kanisa ambalo Yesu alisema atalijenga ni ufalme amba o ulishatabiliwa na manabii tangia awali katika Agano la Kale.

Dibaji

I. Kuna mambo ya kutatanisha ukipungukiwa na. Ukweli, kubaini kweli kutoka kwenye uongo kutenganisha ngano na makapi. Kufahamu ukweli kati ya mafundisho ya uwongo.

II. Watu wengi husema, na hasa madhehebu kuwa kuna makanisa mengi nawajenzi wengi wamewataja hatawajenzi wenyewe ni watu. Lakini Kanisa la Bwana linaamini kuwamjenzi ni mmoja tu, ni Yesu pekee. Pia hata baadhi ya washiriki wa kanisa huamini hivyo lakini siyo hivyo sababu wanapinga ukweli wa neno la Mungu. Mt. 16:18.

- a. Kanisa ni la Yesu tu.
- b. Mjenzi ni Yesu tu.
- c. Mwenye jina la kanisa ni Yesu tu.

III. Jambo la kushangaza watu tumefikiri kuhusu kanisa na kutoa jibu nje ya maandiko tusifikiri mawazo yetu hapana. Isa. 55:8.

IV. Tuone mwanzo wa Kanisa. Mdo. 2:37. Wakiwa pale Yerusalem.

V. Kansia lilipoanza halikufurahia kufa. Bali lifurahia kukua kwa kanisa kila siku. Mdo. 2:47.

- a. Kanisa liliongezeka.
- b. Washiriki walikuwa na hali ya kujitoa.
- c. Waliuza mashamba, viwanja, wakapeleka kwa Bwana.
- d. Wakawa na umoja.
- e. Walifanya kazi ya Bwana.
- f. Waka jali yatima na wajane. (Yak. 1:27)
- g. Walipendana. Hayo walifundishwa na mitume. Kutokana na maombi ya Yesu. Yoh. 17. Akisema wawe na ummoja si hawatu bali na watakawomwamini yeeye.

VI. Sisi wahubiri wa Kanisa la Bwana tusipofundisha haya makusanyiko yata- kufa mara moja. Tuone makusanyiko ya Korintho, 1 Kor. 16:16. Waliwasaidia wenzao wa kule Yerusalem. Sisi pia tuna wajibu kufundisha washiriki wajue.

- a. Kanisa au kusanyiko lisilowajibika limekufa. Hata kama lina watu.
- b. Umoja.
- c. Kutoa.
- d. Kuhubiri.
- e. Kujali wengine.

f. Imani yan-wito-wao-ubatizo wao. Efe. 4:4, Mt. 17:1, 1 Kor. 16:16, Yak. 1:27.
Itafutwe tiba lifufuke.

VII. Kanisa lazima liwe na maono siyo maono; ya ndoto au miujiza bali ya kukua kwa kazi ya Bwana.

- a. Awe na maono mhubiri.
- b. Wawe na maono washiriki.
- c. Tuwafundishe wafanye kazi.

VIII. Kusanyiko lisilokua basi kuna sababu mhubiri achunguze chanzo cha sababu mapema.

- a. Mtoto asipokua anahitaji lishe.
- b. Pengine ni kilema.
- c. Basi apewa tiba.
- d. Ndivyo hata kusanyiko, lilivyo.

IX. Kila mhubiri awe macho kwa kazi ya Bwana Mungu, atubariki tupate uzima wa milele.

Maelezo

Kanisa linaonekana tangia utabiri wa manabi wa kale. Yoeli aliona kansia ni kama roho akimwangukia, Yoeli 2:29. Liganisha. Mdo. 2:16. Amosi aliona kama maskani ya dari lililobomoka kujengua, Amos 9:11-12. Liganisha, Mdo. 15:13-18. Yeremia aliona kanisa kama Agano Jipyala Bwana, Yer. 31:31; 32:31. Limeandikwa katika mioyo ya watu. Isaya aliona kanisa kama Nyumba ya Bwana, Mika 4:1, Isaya 2:1-4.

Mwisho

Kanisa hali kuanzishwa kwa bahati mbaya likikuwa ni mpango wa Mungu na kusudi hadi milele. Yesu ndiye kichwa cha kanisa na ni Mwokozi, Efe. 5:23-25. Na kanisa litapelekwe na Yesu mbiguni akija mara ya pili, 1 Kor. 15:24.

Asante: Amos Kisulumi.

Kanisa Linaloteseka

2 Thes. 1:3-9.

Kanisa siku hizi kama lilivyokuwa lile la karne ya kwanza, litapata mateso ndani na nje.

Utangulizi

1. Kwamba Kanisa la Agano Jipyä liliteswa kuanzia mwanzo wake ni ukweli usioweza kupingwa.
 - a. Mitume waliteswa kwa ajili ya kweli, Mdo. 4:1-22; 5:17-41.
 - b. Kanisa liliteswa kwa ajili ya kweli, Mdo. 8:1.
2. Kuhusu kanisa.
 - a. Philipi Sahaff alisema, “....lakini kanisa la wote la Kristo katika utakatifuwake ni imara mno (zaidi) ya milango ya kuzimu, litabadili mawazo yake ya duniani kwa ajili ya vazi la bibi arusi wa mwanakondoo, na kuinuka toka hali dhalili na kuwa katika hali ya kukuzwa na kutukuzwa.” Watu binafsi lazima wateseke (au kuudhiwa) kwa ajili ya kweli, 1 Pet. 4:12-13.

Kujadili

- I. Kanisa liliteswa (liliuamizw a) katika mapambano na dini ya Kiyahudi.
 - a. Dini ya Kiyahudi ilikuwa ndiye adui dhahiri wa kanisa.
 1. Kulikuwa na juhudzi ya kudumu kuhusisha sheria za musa katika kanisa, na hasa jadi (taratibu) ya kutahiri, Mdo. 15.
 2. Lakini injili ilitimiliza sheria za mungu na kuziondoa; zikagongomewa msalabani, Efe. 2:14,15; Kol. 2:14.
 3. Sura 28 za kitabu cha Matendo zimejaa matukio yanayothibitisha kuwako kwa matatizo katika utaratibu wa Wayahudi.
 - b. Mwanzilishi wa kanisa (Mt. 16:18) ni kweli alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu, Isa. 53.
 1. Kanisa halikutokana na kukua kwa dini ya Kiyahudi.
 2. Kanisa lilikuwa ni utimilifu wa unabii wa zamani, nyakati za mababa na Musa, Mt. 24:34.
 - a. “Kizazi” kuainishwa. Kipindi, wakati au taifa imara.
 - b. Thayer-kipindi au wakati uliotumika, au watu wanaoishi wakati mmoja.
- II. Kanisa liliteswa na falsafa ya Kiyunani.
 - a. Kanisa likwanza na kuishinda falsafa iliyokuwa imeanzishwa Athene, Mdo. 17.
 1. Wastoiko, Mdo. 17:18.
 2. Waepikure o, Mdo. 17:18.

3. Wale Wakolosai wenyе mafundishо ya uasi, Kol. 2:8.
 b. Fabafa ya wanadamу haikuwa (na haiko) sawa na ufunuo wa Mungu,
 1 Kol. 2; 13; 1:18-29; 2:1-5, Kol. 2:8.

- III. Kanisa liliteswa (liliudhiwa) katika mapambano na upagani.**
- Rumi ilipofahamu kuwa kanisa halikuwa na maendeleo ya dini kiyahudi mzozo mkali ulitokea, Ufu. 6:9-11; 20:4.
 - Kusudi la upagani lilikuwa ni kufutilia mbali jina la “Kristо” na “ukristо” kwenye uso wa dunia.
 - Upagani uliruhusu umati wa miungu, Mdo. 17:22, 23.
 - Ibada ya sanamu ilienea katika maisha ya wenyeji wa Rumi.
 - Kumwabudu mfalme kulikuwa ni lazima, lakini kanisa lilipinga.
 - Kanisa lilitfundisha kwamba watu wote walikuwa sawa, hilo livilunja tofauti kati ya bwanan na mtumwa.
 - Kanisa liliwafikia watu wa kawaida, hilo liliwachukiza wapagani.

- IV. Kanisa linaudhiwa (linateswa) na kutokea kwa mitindo au miundo wakati uliopita na uliopo ipo ile ambayo kwa lugha ya kiingereza hutajwa kwa kumalizikia na “ism”.**
- Modernism -mafundishо yenye kuhusisha mambo ya falsafa ya sayansi kwa jamii ya kisasa.
 - Liberalism -mafundishо yenye kuruhusu uhuru wa mapokeo ya jamii.
 - Denominationalism -mafundishо yenye mwelekeo wa kutenganisha imani.
 - Atheism -mafundishо yanayodai kuwa hakuna Mungu.
 - Skepticism -tabia ya kuwa na mashaka katika jambo au imani.
 - Agnosticism -mafundishо kwamba kuna umilele wa aina mbili, moja ya ulimwengu wa kiroho, huu wa pili hufikiwa tu kwa kujinyima na kuwa ufahamu wa juu kuzidi huu hapa duniani.
 - Humanism -utaratubu wa mawazo au maisha, ambao kilicho muhimu ni matakwa ya vitu vya duniani.

- V. Kanisa linaudhiwa katika mapambano na ndugu wapotofu.**
- Ndugu wapotoshaji wasipewe jukwaa lolote, Gal. 2:1-5.
 - Mdo. 10:1-3.
 - 2 Kor. 11:24-28.

Mwisho

- Wote wanaoishi maisha ya utauwa wataudhiwa (au kuteswa) 2 Tim. 3:12.
- Kanisa lilikuwa ni “ishara ya tahadhari” katika kitabu chote cha Matendo.
- Lakini Yesu alisema, “milango ya kuzimu haitalishinda” Mt. 16:18.
- Kanisa leo linaudhiwa (linatesek a) kutoka ndani na nje, lakini Mathayo 24:35, panadhihirisha ukweli leo kama vile palivyodhihirisha ukweli wakati ule aliposema Yesu Kristо, “neno halitapita”.

Asante : B. J. M. Kulanga

Walimu Wa Uongo Kanisani

Utangulizi

1. Walimu wa uongo wamesumbua ukweli na daima watafanya hivyo.
 - a. Kanisa linapaswa kufahamu namna ya kukabiliana nalo kibilia.
2. Katika sehemu nyingi palipo na kilicho halisi, hufuatwa na cha kughushi.
 - a. Kama hakuna kilicho cha thamani, hakuna faida kukuza moyo wa kuiga.
 - b. Ukweli hauna bei (Mith. 23:23) kwa hiyo hauwezi kuleta isiyokweli.
 - c. Yehova anafahamu kwa ukweli wake utamwachisha ibilisi kuleta uongo wake.
 - d. Agano la Kale linaonya kuhusu manabii ya uongo, Yer. 8:8; Eze. 13:9; 22:26, 28.
3. Israeli ilivamiwa na manabii wa uongo.
 - a. Isingelikuwa hivyo, pasipo ukweli hakutakuwa na uongo.

I. Walimu wa uongo katika kanisa.

- a. Maonyo ya Agano Jipy.
 1. Tunakuta katika kurasa za Agano Jipy maonyo kadha wa kadha kuhusu walimu wa uongo, Mt. 7:15; 24:11; 2 Pet. 2:1; 1 Yn. 4:1; Mdo. 20:30.
 2. Unabii ulitimilika na walimu wa uongo walitokea kati ya watu wa Mungu katika karne ya kwanza.
 - a. Kulikuwa na walimu wa uongo katika Antiochia ya Shemu, Mdo. 14:26; 15:1.
 - b. Kulikuwa na walimu wa uongo kaitka Kanisa la Galatia, Gal. 1:7-9.
 - c. Kulikuwa na walimu w uongo katika Kanisa la Korintho, 2 Kor. 11:4.
 - d. Kanisa lililokuwa efeso lilisumbuliwa na walimu wa uongo, Ufu. 2:1, 2.
 3. Tunahitaji kuangalia kwa makini shauri la mitume kuhusu walimu wa
 - a. 2 Kor. 11:13-15; Fil. 3:2; 1 Tim. 4:1-3.
 - b. Zingatia mambo kadhaa haya.
 - 1) Kwanza, mitume hawakuacha kuwasema kwa sababu ya upendo wa kina waliokuwa nao kwao.
 - a) Kwa kweli ukweli upendo wa kweli utatufanya tuwafunue wale wanaotaka kuliharibu kanisa, Rum. 16:17.
 - 2) Pili, mitume walikuwa wazi kwa kuwataja aina ya walimu wa uongo.
 - a) Hakuna faida yejote kutaja uwezekano wa walimu wa uongo.
 - (1) Tunapaswa kuwafahamu ni akina nani na kufahamu ni nini wanacho kifundisha, 1 Tim. 1:19, 20.
 4. Kuna walimu wa uongo kati ya wale wanaotaka kuurudisha ukristo wa Agano Jipy.

Kipindi cha Ukristo

1. Walimu wa uongo wa karne ya kumi na tisa walisababisha ukweli kuharibika na kuzia

- wale waliokuwa wakitaka kurudisha kielelezo cha Agano Jipy.
2. Walimu wa uongo wa karne ya ishirini wanafanya vile vile.
 - a. Zingatia maneno ya Daudi, Zab. 55:21.
 3. Tunapaswa kuelewa kuwa kutakwako na watumishi wa uongo na walimu wa uongo katika kipindi.
 - a. Tunapaswa kukabiliana na walimu wa uongo leo katika kanisa kwa njia iliyosawa na ile Daudi, Isaya, Danieli, Petro, Paulo na Yesu waliyokabiliana nao.
 4. Tunapaswa kupenda na kuwa tayari kuwapinga walimu wa uongo, Eze. 3:5-9.
 5. Tunapaswa kuwa tayari kutoa jibu kuhusu tumaini tulilo nalo ndani yetu, 1 Pet. 3:15.
 6. Tunapaswa kuchukia kila njia potofu, Zab. 119:104, 128.

Hatamisho

1. Ukweli daima utaleta kughushi kwa wale wasio upenda.
2. Walimu wa uongo daima wamejaribu kugeuza ukweli wa Mungu.
3. Walimu wa uongo huvunja mwili wa kristo bila huruma.
4. Walimu wa uongo wnapaswa kupingwa na kuwekwa wazi, Yuda 3,4.

Asante: Robert Stapleton

Je, Biblia Ndiyo Yenye Mamlaka Katika Mwongozo Wa Biblia?

Warumi 6:17

I. Tunatakiwa kufuata nyayo za nani? Za mwanadamu au za Mungu? Mt. 15:9.

a. Ni lazima tujinyenyewekeze mbele za Mungu?

1. Mathayo 7:21.

2. Yohana 15:14.

b. Ikubali Biblia bila maswali kwa kuwa ni yenye mamlaka yote.

1. Yeremia 10:23.

c. Mwanadamu anahitaji mwongozo ambao ni Biblia.

1. 2 Petro 1:21.

2. 1 Petro 4:11.

3. 2 Tim. 3:16,17.

d. Sasa tuangalie mwaongozo wa vipindi vyote vitatu.

II. Kipindi cha mababu, Waebrania 1:1.

a. Je, Mungu alikuwa na mpango “mwongozo” kwa watu waliokuwepo kipindi hicho?

1. Maelekezo maalum juu ya kujenga safina.

a. Mwanzo 6:5, watu wabaya.

b. Mwanzo 6:3, kuangamia kwa dunia.

c. Mwanzo 6:14, maelekezo maalum.

1. Nuhu alifanya yote, Mwanzo 6:22.

2. Je, Kulikuwa na mwongozo?

a. 1 Petro 3:20.

III. Kipindi cha Musa, Yohana 1:17.

a. Miezi mitatu baada ya kutoka Misri, walifika katika Mlima Sinai, Kut. 19:1.

1. Kutoka 19-20, Mungu alitoa amri.

b. Sheria kwa wana wa Israeli, Kutoka 34:27.

c. Je, walikuwa na mwongozo wa sheria?

1. Kutoka 25:27.

IV. Kipindi cha Kristo, Yeremia 31:31-34.

a. Kinatofautiana na vipindi vile viwili.

1. Sheria imeandikwa mionganoni mwetu, Ebr. 8:10.

b. Kilianza baada ya kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo.

1. Ebr. 8:6-13; 9:15-17.

c. Je, Agano Jipywa ni mwongozo wa kipindi cha Kristo?

1. Kol. 2:14 - Sheria ya Kale iliondolewa.

2. Mt. 28:18 - Yesu ana mamlaka yote.

3. Wote tupo chini ya mamlaka hayo.

4. Kichwa cha kanisa ni Kristo, Efe. 1:22-23.

5. Alinunua kanisa kwa damu, Mdo. 20:28.
6. 1 Kor. 13:10; Efe. 4:12-13; Yuda 3; 2 Tim. 3:16-17.

Asante: Heath Stapleton

Kazi ya Kanisa

1 Petro 2:5, 9.

Kanisa linapaswa kutangaza utukufu wa Mungu aliye waita kutoka gizani.

Utangulizi

1. Maana kamili ya neno “kazi” ni lengo linalo fanya kanisa kuwepo.
 2. Kila kitu kilicho wekwa na Mungu kina kazi kamili “ama” maalum, Efe. 2:10.
 3. Kanisa linayo kazi ya kufanya.
 - a. Kazi ya kanisa sio kukaa starehe mpaka mwisho wa safari.
 - b. Sio kama waliomo merini bali kama waliomu katika mtumbwi.
- I. Mambo ambayo sio kazi ya kanisa.
- a. Si kufanya kazi kama dunia inanyotaka, 1 Yoh. 2:15-16, 1 Pet. 1:13-14, 17-22.
 1. Injili sio agizo la mwanadamu, Rum. 1:16.
 2. Mpango wa mungu usibadilishwe, 2 Pet. 1:20-21.
 3. Kristo hakufa ili awapendeza wanadamu au kuwa furahisha, 1 Kor. 15:3, Rum, 14:8-9.
 4. Hakuna utaratibu wa kuwa furahisha, Mk. 12:1-7.

II. Kazi za kanisa.

- a. Kutangaza fadhili za Mungu, 1 Pet. 2:9.
 1. Tuepuke tamaa za mwili, 1 Pet. 2:11.
 2. Kanisa linataki wa litangaze bila kupu mnzika, Efe. 3:9-10; Kol. 1:26-28.
 3. Kazi hiyo ni pamoja na mshiriki mmoja moja.
- b. Hata vitu vilivyoumbwa vina kazi ya kutangaza mambo ya utukufu.
 1. Mbingu, Zab. 19:7.
 2. Anga.
 3. Viumbe hivyo havifanyi tofauti na Mungu alivyo kusudia.
- c. Mungu ameliweka kanisa liwe mwangaz a kwa mambo kama yafuatayo.
 1. Lione kane na watu, Mat. 5:15-16.
 2. Na hekima, Efe. 5:15.
 3. Liwe na uaminifu, Mat. 5:48; Rm. 8:14.
 4. Liwe ni kama kikundi cha askali cha kulinda amani, Eze. 3:17; Yer. 6:16-17.
- d. Kanisa lazima lifanye kazi ya kutoa sadaka, ikiwa ni pamoja na kila aliyeokolewa.
 1. Kutoa miili pamoja na mali zenu, Mdo. 2:44-45; 4:32-35.
 2. Maisha, mali, kabidhi ukakae mahali paraha, Mat. 6:19-21.

Mwisho

1. Kila mkristo lazima afanye kazi ye ye kama ni kanisa akiwa bado yuhai, Yoh. 15:1-6.

Asante: Edson J. Mwalugamba

Kanisa Na Ushirika Na Madhehebu?

Utangulizi

1. Katika miaka kadhaa iliyopita mengi yamesemwa kuhusu ushirika katika madhehebu.
 - a. Marekani kumekuwa na mengi ya yale yaliyoitwa “mikutano ya umoja” ikifanyika ili kulileta Kanisa la Bwana katika ushirika na madhehebu.
2. Neno “ushirika” (sugkoinoneo, katika Kiyunani) humaanisha “pamoja au na ongeza kawaida.” Hivyo, kutumia katika ushirika na au kushirikia na na mtu mwingine.
3. Neno “madhehebu” linahusu “tabaka, aina fulani, mahubiri, shughuli au kikundi cha dini chenye mambo maalum yanayokipambanua kikiundi hicho (Kamusi ya Baker ya Theolojia u.k. 163).
 - a. Kwa hiyo tunahitaji kujadili kama sisi kama Kanisa la Kristo tunahitajika kuwa pamoja na au kushirikian a katika shughuli ambazo zinayahusu makundi mbali mbali ya dini, yanayoshikilia mambo maalum yanayoyapambanua.

I. Tunaweza tukawapan ga kitabaka namna gani watu wa Mungu?

a. Ni watu walioitengwa.

1. Mungu alimtenga Nuhu kutoka katika ulimwengu wa zamani kwa ghalika, Mwa. 6.
2. Ibrahamu aliitwa atoke katika nchi yake na watu wake, Mwa. 12; Mdo. 7:1-4.
3. Waisraeli waliitwa watoke Misri (Hos. 11:1) kuwa taifa takatifu kwa milki ya Mungu, Kut. 19:5, 6.
4. Mungu aliwaita watu wake waondoke katika machafuko ya Babeli, Isa. 52:1.

b. Kanisa ni “walioitwa kwa kutengwa”.

1. Neno “kanisa” katika Kiyunani cha Agano Jipyä ni “ekklesia” kutokana na “ek” nje; na “kaleo” kuitwa.
2. Kwa hiyo kuwa “umeitw a” ni kujibu wito wa injili, 2 Thes. 2:14.
3. Wakristo wanatakiwa kudumisha hali ya kutengwa, pia utakatifu mkamilifu, 2 Kor. 6:14-7:1.
4. Hiyo inawafanya watu wa Mungu “watu maalum” (milki ya Mungu), Tito 2:14; 1 Pet. 2:9, 10; Kut. 19:5, 6.

c. Kanisa la Bwana sio kikundi cha dini (madhehebu).

1. Wayahudi wenye madhehebu walidhani kuwa kanisa lilikuwa ni dhehebu lingine, Mdo. 28:22.
2. Si jambo la ajabu kama watu leo wanadhani Kanisa la Bwana ni kikundi cha dini au dhehebu.
3. Kanisa -mwili wa Bwana-lilikuwa kamili, lote na timilifu, Efe. 1:22-23.
4. Litaku wa hilo hilo leo tunapotimiza vipimio vitakatifu na kudumisha kutngwa kulikoshaguliwa na Mungu.

II. Je, Kanisa la Kristo linaweza kushirikia na dhambi na makosa na kikadumu katika kutengwa?

- a. Giza la maadili na kiroho (la mwili na kidini) ni dhambi.
 - 1. Tusiwe na ushirika na matendo ya giza yasiyo na matunda, Efe. 5:11.
 - 2. Tunatakiwa “tutoke kati yao na kujitenga”, 1 Kor. 6:17.
 - 3. Tunatakiwa kuenenda katika nuru maana yeye ni nuru, 1 Yn. 1:5-7.
 - 4. Tusifanye makosa au kupita mpaka wa mafundisho ya Kristo, 2 Yoh. 9-11.
- b. Umadhehebu ni dhambi kwa sababu unapingana na kipimo kitakatifu.
 - 1. Unapinga (kukataa) sala ya bwana kwa ahili ya umoja, Yn. 17:11, 21-23.
 - a. Bwana hakuomba kwa ajili ya ushirika tu, Yn. 17:23.
 - b. Neno lina sifa kamili kuamini na namna ya kuamini ili tuwe kitu kimoja, Yn. 17:21.
 - 2. Umadhehebu ni kuwa katika vikundi nya dini na nya kimwili.
 - a. “Kunena mamoja hakuwezi kumaanisha kulegeza ukweli,” 1 Kor. 1:10.
 - b. Umona katika tofauti ni wa kimwili na kuenenda kwa kufuata mwanadamu (watu), 1 Kor. 3:3, 4.
 - 1) “Wawili waweza kutembea pamoja, isipokuwa wamepatana?”
 - 3. Umadhehebu “hufanya makosa” au kupita mpaka wa mafundisho ya Kristo, 2 Yoh. 9-11.
 - a. “Mafundisho ya Kristo ni zaidi ya kukiri Uungu wake,” 1 Kor. 15:1-4.
 - b. Kuna amri za kutii, 2 Yoh. 6; Mdo. 2:42.
 - c. Sio tu madhehebu wanapita mpaka wa mafundisho, bali pia wanaacha mafundisho (yaani hawashikamani nayo).
 - d. Hatuwezi kuwa na Mungu wakati tunawapa nguvu ya ushirikiane, 2 Yoh. 11.
 - 4. Umadhehebu unakataa “kuwaangalia na kujiepusha na wale waliomo katika upotofu,” Rum. 16:17.

Hatimisho

- 1. Ni lazima tudumish e kujitenga kulikochaguliwa na Mungu.
 - a. Kama watu wa mungu wa zamani, ndivyo tulivyo, tumeitwa tutoke katika ulimwengu wa giza ili kuonyesh a dhahiri nuru ya ajabu ya Mungu, 1 Pet. 2:9, 10.
 - b. Ingawa katika udhaifu wetu wa kibinadamu, tuna matatizo katika kufuat a kielelezo kitakatifu, 1 Kor. 1:2, 8, 9.
 - c. Tusiwe na “hila wala kunyanzi au cho chote cha namna hiyo,” Efe. 5:27.
- 2. Kushiri makosa ni kuwa mkosefu.
 - a. Dini potofu ni msingi wa mambo ya sanamu.
 - b. Hao hawana Mungu, na Mungu hatakuwa nao, 2 Yoh. 9; Mt. 7:23.

Asante : Robert Stapleton

Kielelezo Cha Kanisa La Agano Jipyा.

Efeso 3:8-11.

I. Daima kunakuwa na kielelezo.

- a. Nuhu, Mwa. 6:14.
- b. Musa, Kut. 25; Ebr. 8:5.

II. Kanisa ni mpango wa Mungu.

- a. Mipango miwili ya Mungu.
 - 1. Kanisa-pasipo agizo la Mungu, hapana amri ya Mungu.
 - 2. Nyumba-Mungu alianzisha mpango wa nyumba na kuweka katika mpangilio.
- b. Pia kanisa ni lazima lilingan e na kielelezo cha, “kusudu la Mungu la milele” (Efe. 3:11) ili tupate rehema za Mungu.
 - 1. Kanisa maskani ya Mungu, Efe. 2:22; 1 Kor. 3:16.
 - 2. Ni lazima tumpendeze Mungu, tusijipendeze sisi.

III. Kanisa limepangiliwa na limekusudiwa milele.

- a. Efe. 3:8-11.
 - 1. Haidhaniwi kamwe kuwa kanisa ni halikujulikana na Mungu.
 - 2. Kanisa ni la milele kama Mungu alivyo.

IV. Kanisa la Agano Jipyा ni utimilifu wa utabiri wa Agano la Kale.

- a. Mungu ndiye aliyekuwa mtabiri wa kwanza, Mwa. 3:15.
- b. Mungu pia alitabiri kwa njia ya “watakatifu wa Mungu”, 2 Pet. 1:21.
 - 1. Musa, Kumb. 18:15.
 - 2. Daudi, 2 Sam. 7:12-16.
 - 3. Isaya, Danieli na Yoeli sura 2 yote yalitimia katika Mdo. 2.

V. Kielelezo kiliweza kufanyika kwa sababu ya Kristo.

- a. Kristo aliquja kufanya mapenzi ya Baba yake.
 - 1. Yn. 17:20.

VI. Kanisa lina kielelezo cha kufuata katika haki ya makubali ano.

- a. Kusikia, Rom.10:17.
- b. Kuamini, Yn. 8:24, Mdo. 8:37, Efe. 5:23, 1 Kor. 15:1-4.
- c. Kutubu, Mdo. 3:19, Lk. 13:3, 5, Mdo. 2:38.
- d. Kukiri, Mdo. 10:32, Mdo. 8:37.
- e. Kubatizwa, Rum. 6:3, 4, Gal. 3:27.

VII. Lina kielelezo katika.

- a. Mahubiri, Mdo. 2:42.
- b. Kutoa, 1 Kor. 16:2.
- c. Kuimba, Kol. 3:16,17.

- d. Kuomba, Mdo. 2:42.
- e. Chakula cha Bwana, 1 Kor. 1:23.

VIII. Linaongozwa na kielelezo kilichotolewa.

- a. Munfu alimkabidhi Kristo, 1 Kor. 15:24.
- b. Kristo ni kichwa, Kol. 1:18, Efe. 5:23.
- c. Wazee, Ebr. 13:7, 12.
- d. Mashemasi, Mdo. 6:1.
- e. Washiriki, Mt. 28:18.
- f. Agizo ni la lazima.

IX. Kanisa la Agano Jipyä linaongozwa na Agano Jipyä.

- a. Sasa ni katika nguvu.
- b. Wote ni lazima wafuate Biblia.

Asante: Heath Stapleton

Sababu Zinazofanya Kanisa Likue

Mdo. 8:4.

Katika Agano Jipya kuna misitari au maelezo ya kutuongoza jinsi ya kukua kwa kanisa mtu hana haki ya kubadili sheria ya Mungu.

Dibaji

1. Tumejaza mawazo mabaya na kutowa visingizio tunaposhindwa kuendeleza kazi ya Bwana.
2. Kitabu cha Matendo kinatuonyesha jinsi neno la Bwana lilivyozidi kuenea, Mdo. 12:24; 6:7.

Maelezo

I. Leo tufanyeje kulikuza kanisa au kuwaokowa watu waliopotea? Kuna sababu kama nne.

- a. Kila mkristo (mhubiri) awe ameongoka (amebadilisha maisha yake kutoka kwa Shetani).
 1. Kuwa kielelezo kwa watu wote, 1 Tim. 1:16, 2 Tim. 1:13.
 2. Kuachana na mambo ya ulimwengu, Gal. 5:19-21.
 3. Kufungua Biblia, 2 Tim. 2:15.
 - b. Kila mkristo atambue ya kuwa bila ye ye kuhubiri injili hafiki mbiguni.
 1. Kazi ya kuhubiri injili ni ya kila mkristo, 1 Thes. 1:7, 2 Tim. 2:2.
 2. Tuhubiri neno la Mungu tu, 2 Tim. 4:2-5, 3:16-17.
 3. Mafundisho ambayo hatuwezi kuthibitisha tuepukane nayo, 1 Tim. 6:3-4; 1 Thes. 5:21.
 - c. Kila mkristo atambue kuwa watu wamepotea na kuwapenda.
 1. Hubiri injili kwa kila mtu, Mt. 28:19-20.
 2. Ni lazima tukue katika ukristo wetu, tusipoku a ni dhambi.
 3. Tukue katika kiroho na kimwili, 1 Kor. 3:1-3.
 - d. Kila mkristo au mhubiri atambua kuwa matumaini yake ni kwenda mbiguni.
 1. Washiriki wote watambue kuwa wanataka kwenda mbiguni.
 2. Kuwafundish a wote neno la Mungu, 1 Tim. 4:6.
 3. Kuhimizana katika kazi ya Bwana, Ebr. 10:24.
- Ii. Tumepungukiwa imani, maono, matumaini na upendo katika kazi ya Bwana.
- a. Sasa basi tuirudie Biblia tufanye kazi ya Bwana, tuwe na madarasa, tuhubiri nyumba kwa nyumba, tufanye mikutano na tuwapende watu waliopotea.
 - b. Tukifanya hivyo itakuwa kama kanisa la kwanza; hawakuacha kufundisha nyumbani mwao, Mdo. 5:42. Ni lazima kila mkristo aokoe kilichopotea, Lk. 19:10, azae matunda, Yoh. 15:16. Lazima awaokoe wengine katika moto kwa kuwanyakua. Yuda 23, mkristo ambaye hajavua utu wa kale, huyo hafai katika kazi ya Bwana,

Efe. 6:10-20. Kazi yake ni kubwa, lakini Mungu ni mkubwa zaidi; pia kazi yetu ni chungu ina thawabu kubwa mno. Na sisi leo tunaweza kukua tukimtanguliza Mungu Bwana wetu katika kazi yake.

Asante: Boaz Kasiba

Kanisa Na Nidhamu

Utangulizi

1. Watu wengi wamesema kwamba nidhamu ya kanisa ni amri iliyosahaulika katika karne ya 20.
 - a. Kutoptaka na tunachokiona kanisani leo inaonekana usemi huo ni kweli.
2. Kama kanisa linatakiwa kubaki safi kama litakiwazvyo, basi nidhamu sahihi ni lazima itendeke.
 - a. Somo letu leo linahusu kujifunza somo la nidhamu ya kanisa.

Jambo lenyewe

I. Viongozi katika kusanyiko.

- a. Katika nidhamu, kama ilivyo katika mambo mengineyo, wazee ni lazima wawe mstari wa mbele.
 1. Ni wajibu wao kulilisha kanisa, Mdo. 20:28.
 2. Ni wajibu wao kuwasaidia walio dhaifu, Mdo. 20:35.
 3. Wanapaswa kuwaangalia wale walio chini ya uangalizi wao, Ebr. 13:17.
- b. Kila kusanyiko, hata kama hawana wazee wa kanisa, linaweza, na ni lazima kutekeleza nidhamu.
 1. Hatuwezi kudai kwamba kwa sababu hakuna wazee wa kanisa basi ni lazima kuruhusu cho chote kuwa ndani ya kanisa.
 - c. Kama kusanyiko lina sifa za kuwa na haki ya kuwako, lina haki ya kujilinda dhidi ya wale wanaotafuta kuyapindua au kuharibu amani yake.
 1. Bwana analitaka kanisa lake liwe safi na lenye kufaa katika utumishi wake.
 - a. Hili ndilo kusudi la nidhamu.

II. Maana ya nidhamu.

- a. Nidhamu ya kanisa hufuatana na mafundi sho, mazoezi, kuadibisha na kukua au maendeleo ya wafuasi wake.
 1. Hatima yake katika hayo yote ni wokovu kamili kwa wale waliomo katika kanisa.
- b. Tusiamini kwamba nidhamu hushughulika na kumwondo mshirika asiyé na mwenendo mzuri.
 1. Kumwondo uwe ni uamuzi tu wakati hatua zote zingine za nidhamu zimeshindwa.

III. Umuhimu wa nidhamu.

- a. Katika kila jumuia yenye taratibu nzuri nidhamu ni lazima isumishwe.
 1. Vinginevyo itavunjika vipande vipande.
- b. Nidhamu hukuza amani na furaha, pia na ufanisi wa mwili, na hukuza tabia ya wote wahusikao.
 1. Fikiria juu ya nyumba isiyo na nidhamu.
 2. Fikiria juu ya jeshi lisilo na jambo hilo.
- c. Makanisa mengi, katika njia yake isiyo na utaratibu, hujali kidogo au

kutojali kabisa mambo ya nidhamu.

1. Hakuna juhudhi yenyeye utaratibu kuelekeza au kuwazoeza washiriki kuwa watenda kazi wenye ufanisi.

IV. Mipango (njia za) nidhamu.

a. Nidhamu ya binafasi.

1. Kila mshiriki ahiangalie kinidhamu.
 - a. Paulo aliutesa mwili wake ili autishe, 1 Kor. 9:27.
 - b. Tumeambiwa tuusulibishe mwili, Gal. 5:24.
 - c. Tuushinde ubaya kwa wema, Rum. 12:21.
 - d. Tusiridishie matusi, 1 Pet. 2:23.
 - e. Uvumilivu wetu na ujulikana kwa wote, Flp. 4:5.
 - f. Tusijilipize kisasi, Rum. 12:19.
 - g. Kuwatanguliza wenzetu, Rum. 12:9,10.
- b. Kanisa kama chanzo cha nguvu.
 1. Kila juhudhi lazima ifanyike kuwendeleza kila mshiriki wa kanisa.
 - a. Kanisa ni ghala la nguvu isiyosemeka.
 - c. Kufundisha na kuonya.
 1. Hakuna anayeweza kukuza maisha ya kikristo bila kuendelea kukua katika ujuzi.
 - a. Wakristo huishi kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu, Mt. 4:4.
 2. Wazee wa kanisa lazima walilishe kundi ili likue, Mdo. 20:28; 1 Pet. 2:2.
 3. Paulo alihitahidi kutafuta kufundisha yale yaliyokuwa na faida, Mdo. 20:20, 35.
 - d. Mazoezi katika utumishi.
 1. Ujuzi peke yake hautoshi.
 2. Maendeleo hultea na mazoezi ya ujuzi.
 - a. Yohana aliwafundisha wanafunzi wake jiinsi ya kuomba, Lk. 11:1.
 - e. Kutia moyo.
 1. Paulo aliwasihii ndugu kuwatia moyo wanyonge, 1 Thes. 5:14.
 - f. Kukaripia na kukemea.
 1. Kukaripia kusilete hali ya kujisikia aliyekaripiwa amemfanya mkarikpiaji afuahie onyo hilo.
 - a. Kusiwe na roho ya kujiona ni bora au tabia ya kujiona, “mtakatifu kuliko”.
 2. Mpango unaostahili humfanya aliyekaripiwa audi kwenye njia upasayo, Gal. 6:1.
 3. Kuna nyakati ambazo karipio la hadhara ndilo kushikiliwa, 1 Tim. 5:10; Tit. 1:13.

V. Hatua ya mwisho.

- a. Wakati juhudhi za kufundisha na kuelekeza, kukemea na kuonya, zimeshindwa kumrudisha mtu kwenye msari utakiwao au mkosaji kumfanya atubu, hatua inayofuata imeelzwa dhahiri ndani ya maandiko.
 1. Katika hali hiyo, hatuna chaguo bali kufanya lili ambalo Bwana ameamuru.
- b. Tafakati 1 Kor. 5:1-7; 2 Thes. 3:6; Tit. 3:10,11; Ufu. 2:20-21.

VI. Jinsi ya kuendelea.

- a. Roho sahihi.
 - 1. Lango la kukamilisha hatua zote za nidhamu ni kumkuza mshiriki katika kutumika kwake kwa hali ya juu kuhusu wokovu wake.
 - 2. Kumtenga mshiriki kutoka katika ni jambo la kuliangalia sana.
 - 3. Mtu na aendelee na sio kushindwa.
- b. Mambo ya mtu binafsi (yasiyojulikana na jumuia).
 - 1. Fikiria Mathayo 5:23-24; 18:15-18.
 - 2. Wajibu wa kuchukua hatua za kusuluuhisha jambo la kikinafsi ni juu ya mkosaji na mkosewa.
 - a. Kama mtu anajua ndugu yake anajisikia kuwa amekosewa, inafaa aende afanye suluhu naye.
 - b. Kama mtu anafikiri amekosewa amwendee aliyemkosea.
 - 3. Kuwe na nia yenye nguvu toka pande zote mbili inayoongoza kwenye shauku ya kujitoa mhanga na kukubali ukweli kuhusu haki na majaliwa yao.
 - a. Tabia hii inapokuwako katiak pande zote mbili, kwa kawaida maafikiano hutokea.
 - 4. Daima tukumbuke maneno ya Yakobo 5:19-20.
- c. Makosa ya hadhara.
 - 1. Kwa hilo tuna maana makosa yanayoathiri mwili mzima, kanisa.
 - 2. Dhambi ya upande wowote (mshiriki ye yote) ambayo inajulikana kiujumla ni dhambi ya hadhara.
- d. Viongozi katika kutenga.
 - 1. Wazee wa kansia, wanapokuwapo, kwa kazi hiyo, wana wajibu kwa mambo hayo yote.
 - a. Ni vema kwa uangalifu na kwa sala walichunguze jambo lo lote waliloletewa.
 - 2. Kama ni kosa la hadhara, matokeo ya uchunguzi ni kulileta kundini.
 - a. Kama mshutumiwa amwpatikana na hatia, na hataki kutubu, watagaze kwamba wametumia uwezo wao wote wa kumrejeza pasipo mafaikio.
 - 3. Wakati hatua hiyo ya mwisho imefikiwa kusanyiko lote likubaliane juu ya jambo lenyewe, 1 Kor. 5:1-7; 2 Kor. 2:2-6.
- e. Kufanya utekelezaji mkamilifu.
 - 1. Mara kwa mara kutenga katika ushiriki kumekuwa na maana ndogo sana au hakuna kabisa.
 - a. Mkosaji hajisikii uzito wa kumtenga huko.
 - b. Tabia yetu mbele ya mtu huyo kabla na baaa ya kumtenga ina tofauti ndogo mno.
 - 2. Mwelekeo huo una hali ya kumfanya mtu aone kanisa limefanya taratibu zisizo na mana yo yote.
 - 3. Aliyetengwa ni vema “aonywe kama ndugu”.
 - a. Hata hivyo, kwenye uhusiano wa kijumuia tuepuke.
 - b. Tusishirikiane naye.
 - c. Tukatae hata kula naye katika hali yo yote itakayoonyesha ushirikiano, 1 Kor. 5:9-11.

VII. Kupinga.

- a. Kupinga kwingi kunakotolewa kuhusu swala la kujitenga katika ushirikiano hakustahili kufikiriwa.
 - 1. Hivyo ndivyo ilivyo kwa sababu ya ukweli kwamba hakuna kupinga kunakoruhusu kwenda kinyume na amri za mungu.
- b. Kile kinachoitwa ni upingaji wa kimaandiko kifikiriwe.
 - 1. Ona Mat. 13:24-39.
 - 2. Ili kuona huu sio upingaji halali ni lazima kuyafikiria maelezo yaliyotolewa na yesu kufuatana na ombi la wanafunzi wake.
 - a. Yesu alipanda mbegu njema.
 - b. Shamba ni ulimwengu.
 - c. Mbegu njema ni wana wa ufalme -yaani washiriki wa kanisa.
 - d. Magugu ni watoto wa ibilisi.
 - e. Adui aliyepanda magugu ni Shetani (Ibilisi).
 - f. Mavuno ni mwisho wa dunia.
 - g. Wavunao -watumishi -ni malaika.
- 3. Hata kwa tafsiri ya namna gani unayoweza kuiweka juu ya mfano huo, ni ukweli kwamba housemi neno hata moja juu ya mbegu njema kutotengwa dhisi ya magugu.
 - a. Lakini inaonyehsa kwamba malaika -wavunaji -wasiyalingilie masuala hayo mpaka ufile mwisho wa wakati.
- d. Hakuna mtu anayeweza kuweka tafsiri ya mfano au usemi wa mfano wa aina yo yote ile, inayopingana na amri ya wazi.
 - 1. Hatuna haki zaidi ya kutangua amri ya wazi kwa kutumia tafsiri zetu kuliko tufanyavyo kwa mapokeo yetu.
 - 2. Tumeamuriwa “kujitenga dhisi ya ndugu ye yote aendaye bila utaratibu.” 2 Thes. 3:6.

Mwisho

1. Ni lazima tujitahidi kulifanya kanisa liwe safi.
 - a. Nidhamu ya kweli itaendelea kufanya juhudili ili kuhakikisha kwamba hilo linatendeka.

Asante: Robert W. Stapleton

Kanisa La Kiaskari

2 Kor. 10:3-5

I. Uaskari humaanisha nini?

- a. Kanisa kupigana kitakatifu “vita vya kiroho”, 2 Kor. 10:3-5.
 - 1. Dhidi ya maovu yote na Shetani, Efe. 6:10-18.
- b. Siyo vya mwili bali vya kiroho; vita vitakatifu kwa Upanga wa Roho, Mat. 10:34.
 - 1. Kila shiriki awe “askari mzuri (mwema)”, 2 Tim. 2:3.
 - 2. “Kupigana vita vyema vya imani,” 1 Tim. 6:12.
 - 3. Simama pamoja naye au kinyume naye, Mat. 12:30.
- c. Uaskari huelezea, “kushughulika na mambo ya vita; kupigana; hamasika kiushambulish aji; akupambana.”

II. Je, kanisa la awali lilikuwa la kiaskari?

- a. Mvuto wao unaonyesha tabia yao mbele za Mungu, Mdo. 17:24-31.
 - 1. Waliwaza kuuwawa, kuteswa, kwa sababu ya tabia yao ya kiaskari.
 - 2. Walimjua Mungu, walipokea, walifundi sha na kupigania tu kwa ajili ya Mungu mmoja, Efe. 4:4-6.
 - 3. Kamwe hakukuwa na sauti isiyo na hakika katika tabia yao ya uaskari.
- b. Lilikuwa la kiaskari kwa sababu lilikataa kubaki kimya.
 - 1. Wote walilihiri, walifundisha wokovu katika jina moja, Mdo. 4:12; 3: 19-22; 2 Thes. 1:7-9.
 - 2. Walikiri kwamba waliamini, Yoh. 8:24.
- c. Lilikuwa la kiaskari kwa sababu lilizipinga njia zingine zote.
 - 1. Liliushindania na kuipigania umoja.
 - 2. Lilipinga kuwa imani moha ni njema tu kama nyingine.
 - 3. Lilishindania kuwa imani halisi ilikuja kwa njia ya “kulisikia neno”, Rum. 10:17.
 - 4. Lilihubiri ile imani moja, kila siku, kila mahali, Mdo. 8:4.
- d. La kiaskari kwa sababu ya nguvu iliyotokea.
 - 1. Liliugeuza ulimwengu (kuipindua ulimwengu).
 - 2. Kuweka bayana kwamba upatanisho ulikuwa katika mwili mmoja, Efe. 2:13-16.
 - 3. Kamwe asilimia ishirini -na-tano ya himaya ya kirumi walikuwa wakristo.
 - 4. Warumi hawakuwe za kuusimamisha (kuuzuia), karne ya nne waliukubali.
- e. La kiaskari kwa sababu ya wakristo wakweli.
 - 1. Wakristo waliishi maisha ya kujikabidhi.
 - a. Waliitoa miili yao iwe dhabihu.
 - b. Walijua vita na walipigana nayo.
 - 2. Walikuwa tayari kufa, Mdo. 21:13.
 - a. Hawakuta ka “kuzuia nafsi zao”. “Walitaka kutoa nafsi zao,” 2 Kor. 5:17-19; Rum. 6:3-5.
 - b. Walikuwa tayari “kubeba msalaba,” Lk. 9:23-24.
 - c. Waliamini, “na tupande mara, tukaitamalaki; maana twaweza kushinda bila shaka,” Hes. 13:30, kwa msaada wa Mungu.

III. Je, leo tupo kiaskari?

- a. Ulimwengu leo haujageuzwa (haujapinduliwa); kwa nini?
 - 1. Hatufanyi mambo yale yale ambayo kanisa la awali lilifanya?
 - 2. Tunafanya mambo yale yale pasipo tumaini?
- b. Tunahitaji nini?
 - 1. Tumaini katika imani yetu!
 - a. Karne ya kwanza: njaa ya kumtafuta mungu, waumini wa kweli, wenyewe ibada na nidhamu ya kweli.
 - b. Leo: je, tupo katika hali hivyo ya juu?
 - 2. Wakristo halisi!
 - a. Karne ya kwanza: walitawanyika, walikufa, ila mmoja alifundisha, wakaishi katika yale waliyoyaamini.
 - b. Leo: twatenda?

IV. Umuhimu wa kansia la kiaskari.

- a. Tunaweza kujifunza kwa kupitia katika ujuzi wa Biblia.
 - 1. Mt. 28:19; Mk. 16:15.
 - 2. Efe. 2:12.
 - 3. Rum. 1:16.
 - 4. Yn. 9:4.

Mwisho

Kama Kristo angukuja leo, washiriki wa kanisa wangkuwa katika hali la kiaskari kuwawezesha kuokolewa? Tungeweza kusema haya kwa Mungu bila kusema uongo, “nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda?” 2 Tim. 4:7.

Asante : Heath Stapleton

Tunajua Sisi Ni Kanisa La Bwana Kwa Sababu...

Robert Stapleton

Utangulizi

1. Agano Jipyä linafundisha wazi kwamba kuna kansia moja, mwili moja wa Kristo, Mt. 16:18; 1 Kor. 10:17; 12:12, 13, 20; Efe. 2:16, 4:4; Kol. 3:15.
 - a. Kwa kuwa Agano Jipyä linazungumzia kamisa moha ni vyepesi.
 1. Hata hivyo, kuonyesha kwa mwenzetu (mtu) kuwa Kanisa la Kristo ni lile moja, panahitaji muda wa kutosha, kujifunza na uvumilivu.
 - b. Kama mtu anani na mawazo ya wazi tutakacho kiangalia leo kitaonyesha kutoka katika Biblia kwamba sisi ni Kanisa la Bwana.

Sisi ni Kanisa la Bwana kwa sababu.....

- I. Biblia ni utaratibu wetu wa pekee wa imani na kutenda.
 - a. Madhehebu ua wanadamu hayatumii Biblia tu.
 1. Badala yake yanatumia kanuni, nidhamu na vielelezo vya wanadamu.
 2. Wanazo “taratibu za imani” za wanadamu, maelezo na mafundisho ya vyama yaliyoundwa na watu.
 - b. Kanisa la Bwana hutumia neno la Mungu tu kuliongoza (kanisa).
 1. Kanuni za wanadamu pamoja amri zao na mapokeo ya wandamu havina nafsi katika kazi na muundo wa uongozi wa Kanisa la Kristo, 2 Tim. 3:16, 17; 2 Pet. 1:3.
- II. Tunawaambia wenyе dhambi nini la kufana ili waokolewe, ndani ya maneno ya watu waliovuviwa.
 - a. Kanisa la Bwana linatumia neno la Bwana katika kuelekeza katika njia ya wokovu.
 1. Kama mwenye dhambi aulizaye si mwamini wa Kristo.
 - a. Tunamlekeza katika maneno ya paulo kwa yule mlinzi wa gereza la Filipi, Mdo. 16:30-33.
 2. Kama mwenye dhambi amekwisha isikia injili na ni mwamini katika Kristo.
 - a. Wote wakoa katika hali inayofanana kama Wayahudi Fulani walivyokuwa Siku ya Pentekoste, Mdo. 2:36, 37.
 - b. Tunawaeleza kuhusu wokovu wao, katika macho ya mtume Petro, Mdo. 2:38.
 3. Kama aulizaye ni mwamini aliye kwisha tubu.
 - a. Ni kama Sauli wa Tarso, Mdo. 22:5-9.
 - b. Tunamweleza analazimik a afanye nini katika maneno ya Anania, Mdo. 22:16.
 4. Kwa kuyaweka pamoja maelekezo ya watu walio vuvuwa wa Agano Jipyä, tunafundisha mpango wa mungu wa wokovu wa mpotevu mwenye dhambi.
 - a. Ili mtu aokolewe, ni lazima aamini, atubu, akiri kwamba Yesu ni Mwana na abatizwe kwa kuzikwa ndani ya maji.
 - b. Kanisa la Bwana linatumia maneno ya wale watu waliovuviwa tu kuwaelekeza Wakristo juu ya jinsi ya kupokea msamaha wa dhambi walizotenda.

- 1) Kama mkristo ametenda dhambi?
 - a) Yuko katika hali ya Simoni, Mdo. 8:13-21.
 - b) Kwa yeye tunarudia maneno ya Mtume Petro, Mdo. 8:22-24.

- III. Kila sehemu ya ibada yetu imewekwa wazi katika Agano Jipy.
- a. Kanisa la Agano Jipy linafunua vitendo vyepesi vitano tu vilivyofanyika kama ibada siku ya Bwana na wakristo wa awali.
 - b. Kanisa la Kristo hufuata hivyo hivyo vitendo vyepesi vitano katika ibada ya leo.
 1. Tunafundisha neno la Mungu, Kol. 4:16.
 2. Tunaimba nyimbo za kiroho, Efe. 5:19; 1 Kor. 14:15.
 3. Tunaomba (kusali), Efe. 6:18; 1 Tim. 2:8.
 4. Tunashiriki Chakula Cha Bwana, Mdo. 20:7; 1 Kor. 16:1, 2.
- IV. Kazi yote tunayoshughulikia imewekea wazi katika Agano Jipy.
- a. Agano Jipy yanafunua maneno matatu ambao kanisa limeamriwa kushughulikia.
 1. Hii ndiyo kazi tunatakiwa kufanya.
 - a. Kuhubiri injili kwa waliopotea katika dhambi au kufanya uinjilisti, Mk. 16:15-16; 1 Tim. 3:15; Fil. 4:15-16.
 - b. Kufundisha na kuwajenga wakristo, Efe. 4:11-16; 1 Kor. 14:26.
 - c. Maneno ya kufanya hisani, Gal. 6:10; Yak. 1:27.
 - b. Tunafahamu kwamba maandiko matakatifu yanahitaji kila kusanyiko la Kanisa la Bwana kujitegemea kimamlaka na hakuna kusanyiko lenye haki ya mamlaka kuvuka yale ya maandiko matakatifu, Kol. 3:17.

Hatimisho

1. Endapo hatushidwi kufikia kiwango au hatuvuki kiwango cha mafundisho ya Maandiko matakatifu katika maneno hayo, tunaweza kujua kwamba sisi ni Kanisa la Agano Jipy, Kumb. 4:2; Gal. 1:6-9.
 - a. Taratibu hizi za msinigi zinahitaji kuhubiriwa kwa upendo, Efe. 4:15.
 - b. Zikifanyika hivyo watu watamgeukia Bwana na Kanisa lake.

Asante : Robert Stapleton